

**OFISI YA RAIS TAMISEMI**  
**HALMASHAURI YA WILAYA YA WANGING'OMBE**  
SHULE YA SEKONDARI MARIA NYERERE,  
S.L.P 812,  
**NJOMBE.**  
**07/12/2020.**

**KUMB NA. MNYGS/JIFF/8**  
**NDUGU**

---

**YAH: KUCHAGULIWA KUJIUNGA NA SHULE HII.**

Ndugu \_\_\_\_\_ ninayo furaha kujulisha kuwa umechaguliwa kuendelea na masomo ya elimu ya sekondari katika shule hii mwaka **2021 “HONGERA SANA”**. Shule hii ni ya kutwa lakini ina mfumo kamili wa Hosteli hivyo wanafunzi wote wanakaa Hosteli. Aidha gharama zote za hosteli ni jukumu la mzazi/mlezi wa mwanafunzi.

**1. MAHALI SHULE ILIPO NA UPATIKANAJI WA USAFURI.**

Shule hii ipo katika Tarafa ya Imalinyi, Kata ya Wangama. Shule ipo umbali wa **Km.47** toka Njombe mjini. **Usafiri:** Kuna usafiri wa mabasi a). Toka Njombe mjini ambapo basi huondoka **saa saba mchana** b). Toka Makambako ambapo basi huondoka **saa saba mchana** na c). Toka Illembula ambapo basi huondoka **saa nane mchana**. Mabasi hayo yote yatakufikisha hadi shulenii.

**2. TAREHE YA KUWASILI.**

Unatakiwa kufika shulenii tarehe **05/01/2021**. Muda wa kufika ni saa **2:00 asubuhi** na mwisho wa kuwapokea watoto ni saa **11:00 jioni**.

**3. ADA/MICHANGO NA VIFAA VYA KULETA.**

- i. Hosteli.....Ths.150,000/=  
**Account No.60601000035–NMB NJOMBE (Maria Nyerere Collection Account).**
- ii. Ujenzi.....Ths.40,000/= (**HII NI KWA WANAFUNZI WOTE WANADOKA NJE YA KATA YA WANGAMA TU**)  
**Account No.60610018107–NMB NJOMBE (Maria Nyerere Sekondari).**  
**NB:** Michango tajwa hapo juu iwekwe benki na tuletewe Pay-in- Slip, waweza lipa nusu yake.  
**HATUPOKEI FEDHA** Mkononi.
- iii. Mchango wa kuwawezesha walimu wa masomo ya sayansi na masomo ya jioni Tsh.15,000/= kwa makubaliano ya kikao cha wazazi (**Aje nayo mkononi**)
- iv. Fedha ya ununuza wa gari la shule **Tsh.20,000** kwa makubaliano ya kikao cha wazazi cha mwaka 2020
- v. Rimu au bunda la Karatasi **A4 (Aje nayo mkononi)**

**4. CHAKULA**

- Mahindi debe 10
- Maharage debe 3
- Mchele kg 20

**NB:** Mazao hayo yaletwe shulenii **NUSU YAKE ambayo ni mahindi debe 05, maharage debe 1 1/2 na mchele kilo 10.** Tunasisitiza michango hii uje nayo wakati wa kuripoti hapa shulenii ili kuepuka usumbufu.

**5. SARE ZA SHULE (AJE NAZO)**

- i. Blauzi nyeupe 2 mikono mifupi
- ii. Sketi 2 ndefu rangi ya orange za marinda 12 kitambaa aina ya **esteem no.1**
- iii. Tracksuit Nyeusi.
- (iv) Sweta mbili rangi ya damu ya mzee yenye mshono wa **V.**

- (v) Viatu vya ngozi nyeusi vyenye gidamu na soli fupi jozi mbili .
- (vi) Gauni Mbili rangi ya damu ya mzee, hizo ni nguo za kushindia.
- (vii) Raba nyeupe aina yeoyote kwa ajili ya michezo.  
**NB:** Mwenye Sketi/Gauni fupi hatopokelewa, Pia mwanafunzi **HATAKIWI** kuja na mavazi mengine nje na alioagizwa.

## 6. VIFAA VYA DARASANI

- ❖ Peni za kutosha
- ❖ Penseli
- ❖ Mkebe
- ❖ Madaftari Makubwa (**Quire -03**) yawe 9 au zaidi.
- ❖ Graph paper
- ❖ Madaftari madogo – 12 (**Msomi**) au zaidi
- ❖ Kamusi (Oxford) Lugha ya kiingereza kwa kiingereza
- ❖ Four figure.
- ❖ Saa 1 (Kimulimuli)

## 7. VIFAA VYA CHAKULA.

Kontena la chakula 1 **rangi ya bluu**, bakuli 1, kikombe 1 cha nusu lita na kijiko 1. Pia vyombo vya udongo haviruhuswi.

## 8. VIFAA VYA KULALIA.

Godoro 2.5 x 6 (**DODOMA**) moja, mto 1 blanketi zito 1 shuka 2 rangi ya pinki lisilofumwa na neti ya mviringo kuzuia mbu.

## 9. VIFAA VYA USAFI BINAFSI NA ZANA ZA KAZI.

- i. Jembe 1 jipya na mpini wake, Ndoo kubwa 1, kwanja 1 na fagio ya mchelewa 1.
- ii. Taulo 1, Kitenge 1, mswaki, dawa ya mswaki, sabuni za kutosha.
- iii. Ndoo lita kumi ya kuogea na kufulia moja **rangi ya kijani** tu.

**NB:** Hakikisha unampatia mwanaao mahitaji yake muhimu **ya kutosha** kama vile **hela ya matumizi kulingana na uwezo wa mzazi**, **Pedi bunda 03**, **Chupi 06**, **Taiti 05**, **Underskirt 03**, **Vibody/vitopu/shumizi 05**,

Kindoo kidogo 01 cha **bluu**, Sabuni miche **05**, Mafuta ya kupakaa ya kutosha, Dawa ya mswaki kubwa.

Unaruhusiwa kuja Kumwona/**kumtembelea** mwanaao na kuona maendeleo yake kitaaluma **KILA JUMAPILI YA KWANZA YA MWEZI** na **SI VINGINEVYO**. Wanafunzi **HAWARUHUSIWI kumiliki wala kutumia simu KABISAAA** mbadala wake mwanaao atafanya mawasiliano yake yote na mzazi au mlezi kupitia walimu kwa siku maalumu zitakazokuwa zimepangwa.

## 10. FOMU ZA KUJAZA.

- (a) Fomu ya taarifa binafsi za mwanafunzi ijazwe kikamilifu.
- (b) Fomu ya Daktari kuhusu afya ya mwanafunzi ijazwe baada ya kupimwa (imeambatanishwa). **NB: Mwanafunzi wetu apimwe katika hospitali ya wilaya na siyo zahanati au kituo cha afya.**

## 11. URAIA.

Mwanafunzi aje na cheti cha kuzaliwa kuthibitisha uraia wake.

**NB: Mwanafunzi atakayebahatika kupata nafasi ya kuhamia katika shule yetu ni lazima aje na dawati la chuma.**

Nakutakia maandalizi mema.

**KARIBU SANA MARIA NYERERE**  
Sungu, R  
**MKUU WA SHULE**

## **MARIA NYERERE SEKONDARI SHERIA ZA SHULE KWA WANAFUNZI**

1. Kuwahi kufika mistarini saa 1:00 asubuhi kila siku za masomo
2. Kukimbia mchaka mchaka 11:30 alfajiri kila siku za masomo
3. Kuhudhuria vipindi vyote vya masomo na kufanya usafi eneo unalohusika kwa kuzingatia muda na ratiba ya shule
4. Usafi wa mavazi, mwili na mazingira ya shule ni muhimu
5. Unatakiwa kuomba ruhusa au kutoa taarifa wakati wowote unapokuwa na shida
6. Hutaruhusiwa kubadili jina
7. Hutaruhusiwa kubadili dini ukiwa shuleni mpaka uthibitisho kutoka kwa mzazi au mlezi wako
8. Kitendo cha kutoroka vipindi wakati wowote hakitavumiliwa
9. Ni lazima kuwa katika sare za shule wakati wote na unatakiwa kufanya hivyo
10. Ni lazima kutii kengele na kufika unapotakiwa mara unaposikia kengele
11. Ni kosa kutetea wahalifu kwa namna yoyote
12. Ni marufuku kuwa na nguo za aina yoyote za nyumbani tofauti na ulizoagizwa na shule
13. Ni marufuku kwenda na chakula au kula chakula ukiwa bwenini
14. Ni marufuku kwenda na kandambili eneo lolote la chakula
15. Kudumisha Nidhamu, upendo na amani kwa wanafunzi, walimu na wafanyakazi wa shule
16. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote
17. Bwenini ni mahali pa kulala marufuku kupiga kelele

**NB:** Mazungumzo yoyote bwenini yawe yenye maana, yanayozingatia maadili ya wanafunzi

### **MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA SHULE**

1. Wizi
2. Utoro
3. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya
4. Uasherati na ushoga
5. Kupiga au kupigana
6. Kuharibu kwa makusudi mali za umma
7. Kudharau bendera ya taifa
8. Kuolewa
9. Kupata mimba
10. Kutoa mimba
11. Kugoma, kuchochea na kuongoza au kuvuruga amani na usalama wa shule na watu
12. Kukataa adhabu kwa makusudi

### **KARIBU SANA MARIA NYERERE**

Sunge, R

### **MKUU WA SHULE**

**OFISI YA RAIS TAMISEMI  
HALMASHAURI YA WILAYA YA WANGING'OMBE  
SHULE YA SEKONDARI MARIA NYERERE,**

**MAELEZO BINAFSI KUHUSU TAARIFA ZA MWANAFUNZI.**

- A: 1. Jina la mwanafunzi:.....  
2. Tarehe ya kuzaliwa:.....  
3. Mahali alipozaliwa (Wilaya):..... (Mkoa):.....  
4. Dini:..... Dhehebu:.....
- B: 1. Jina la mzazi/mlezi:.....  
2. Kazi ya mzazi/mlezi:.....  
3. Anuani ya mzazi/mlezi:.....  
4. Namba ya simu ya mzazi/mlezi:.....  
5. Mahali yalipo makazi ya mzazi/mlezi:  
    Mkoa:..... Wilaya:.....  
    Kata:..... Kijiji:.....
- C: Majina ya ndugu wengine wanaohusika na malezi ya mwanafunzi huyo  
1. Jina la ndugu:.....  
    Anuani:..... Simu:.....  
  
2. Jina la ndugu:.....  
    Anuani:..... Simu:.....
- D: Anuani ya serikali ya kijiji ambacho mzazi/ mlezi wa mwanafunzi anaishi  
1. Jina la Mtendaji wa kata/kijiji .....  
    Kata/Kijiji cha:.....  
    Anuani:.....  
  
2. Jina la Mwenyekiti wa Kijiji:.....  
    Kijiji cha:.....  
    Anuani:.....  
    Simu:.....

**ZINGATIA: Fomu hii ijazwe taarifa sahihi**

**KARIBU SANA MARIA NYERERE**  
*Sungu, R*  
**MKUU WA SHULE**

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA  
MINISTRY OF EDUCATION, SCIENCE AND TECHNOLOGY

MARIA NYERERE SECONDARY SCHOOL,  
P.O. BOX 812,  
NJOMBE.

TO:  
THE MEDICAL OFFICER

---

---

---

**RE: MEDICAL EXAMINATION**

Please examiner.....

As to her fitness for perishing further education at this school.

1. Hemoglobin .....
2. P.V. Bleeding .....
3. (b)Hearing.....
4. Blood Pressure.....
5. Urine for sugar and Pregnancy test.....
6. Stool for routine examination.....
7. Asthma.....
8. Skin diseases.....
9. Leprosy.....
10. Epilepsy .....
11. Pulmonary tuberculosis .....
12. Deformity .....
13. Mental problem.....

**COMMENTS:-**

---

---

---

I certify that above is fit/unfit to pursue her lesson as required.

Signature .....

Designation.....

Date ..... Station .....